



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANA
OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOA ZA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA KAHAMA**



Kumb.Na KMC/F.20/10/75

09 Agosti, 2024

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama anapenda kuwatangazia Wananchi wote wenye sifa, nafasi Arobaini na Moja (41) za Ajira ya Muda ya wakusanya Mapato katika Halmashauri ya Manispaa Kahama.

SIFA ZA MWOMBAJI

- i. Mwombaji awe Raia wa Tanzania.
- ii. Awe amehitimu Kidato cha Nne na kuendelea.
- iii. Awe na Mdhamini mwenye mali isiyo hamishika.
- iv. Awe Mwadilifu na ambaye hajawahi kukutwa na hatia Mahakamani.
- v. Awe na uwezo wa kufanya kazi kwa kujituma bila kusimamiwa.
- vi. Awe tayari kufanya Kazi katika Kata yeyote kwa kipindi kisichopungua Mwaka Mmoja.
- vii. Awe na Umri wa kuanzia Miaka 18 hadi 45.

KAZI NA MAJUKUMU


1. Kukusanya Mapato ya Halmashauri ya Manispaa Kahama

MAMBO YA JUMLA YA KUZINGATIA.

- i. Nakala ya Cheti cha Kidato cha Nne na kuendelea.
- ii. Waombaji waambatishe Vivuli vya Vyeti vya Elimu vilivyothibitishwa na Wakili, maelezo binafsi (CV), Nakala ya Cheti cha kuzaliwa.
- iii. Katika barua ya maombi, weka Namba yako ya simu inayopatikana muda wote.
- iv. Barua zibandikwe picha mbili (2) - Passport size.
- v. Waombaji watakaokidhi sifa na vigezo watajulishwa tarehe ya usaili.
- vi. Maombi yote yaambatane na barua za Wadhamini Wawili zinazoonesha Mali zisizohamishika.
- vii. Mwisho wa kupokea maombi ni **20/08/2024** saa **9:30** alasiri.
- viii. Mwombaji aambatanishe cheti kingine chochote cha mafunzo ya ziada kama anacho.
- ix. Maombi yote yaelekezwe Ofisi ya Mkurugenzi Manispaa ya Kahama kwa Anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi wa Manispaa,
Barabara ya Boma,
S.L.P 472
KAHAMA

Limetolewa na:


Masudi S. Kibetu

MKURUGENZI

HALMASHAURI YA MANISPAA

KAHAMA

MUNICIPAL DIRECTOR
KAHAMA MUNICIPAL COUNCIL
P.O. Box 472
KAHAMA